


Huduma za Kikristo za Tony Alamo
Jarida la Dunia
Yerusalemu Mpya
Makanisa Ulimwenguni Kote
Mchungaji Tony Alamo | Taifa la Kikristo la Alamo | Toleo 13600



*Mchungaji Tony Alamo akibatiza mwokovu katika bahari ya Pacific*

# USHINDI DHIDI YA PONOGRAFIA!

**Na Tony Alamo**

**Zaburi 119:9-16 (BETHI): "Jinsi gani kijana aisafishe njia yake? Kwa kutii, akilifuata NENO LAKO. Kwa moyo wangu wote NIMEKUTAFUTA, usiniache nipotee mbali na maagizo YAKO. Moyoni mwangu nimeliweka NENO LAKO, nisije NIKAKUTENDA dhambi."**

**"Ee BWANA umehimidiwa, nifunze amri ZAKO. Kwa midomo yangu, nimezisimulia hukumu zote za kinywa CHAKO. Nimeifurahia njia ya shuhuda ZAKO** kana kwamba ni mali nyingi. Nitayatafakari mausia YAKO, nami nitaziangalia njia ZAKO. Nitajifurahisha sana kwa amri ZAKO. Sitalisahau NENO LAKO."

Zaburi 120:1 inasema hivi, "Katika shida zangu nalimlilia BWANA, naye AKANIITIKIA." Ee BWANA, uiponye nafsi yangu kutokana na Ponografia. Ponografia ni uongo!

Kunalo tumaini la ukombozi kutokana na ponografia ndani ya BWANA na NENO la MUNGU. Tuko katika nyakati za mwisho na shetani anajua kwamba muda wake ni mfupi.[1] Ana hasira nyingi na ndiyo sababu anazidi kutupa mishale kwa wateule na wale ambao wangependa kuwa wateule, wale ambao wangependa kuwa huru kutokana na "mishale ya mtu hodari iliyochongoka, pamoja na makaa ya mteremu" (Zaburi 120:4).

Sote tumeitwa na MUNGU kupigana na shetani. Lakini, vita ambavyo[2] haviishi ukitaka afueni ya kila siku kutokana na mshale huu wa ponografia utokao kwa Ibilisi ambaye angependa uishi naye milele Kuzimu ukichomeka kwenye lava inayochemka ya salfa na kiberititi kule Jehanamu.[3] Lakini, ni vipi waume na wake wa kizazi hiki wataweza kumshinda shetani na silaha hii yenye nguvu ya mawazo machafu ya uchi na usinzi, ambayo ni ponografia?

Katika Zaburi 119:9 (BETHI), Daudi anauliza swali hilo hilo: "Jinsi gani kijana [mwanamke] aisafishe njia yake? [Anatupa sisi sote njia ya pekee ambayo ni NENO la MUNGU.[4] Na jibu lake ni:] Kwa kutii, akilifuata NENO LAKO. Kwa moyo wangu wote nimekutafuta, usiniache nipotee mbali na MAAGIZO YAKO. [Na hapa ndipo kuna siri kuu:] Moyoni mwangu, nimeliweka NENO LAKO, nisije NIKAKUTENDA DHAMBI. EE BWANA umehimidiwa, nifunze AMRI ZAKO. [Kariri maneno haya kila wiki. Zaburi sio hadithi tu, bali ni uwezo wa MUNGU wa kukusaidia wewe kumshinda shetani!

*(Inaendelea ukurasa wa 2)*

**1** Ufu. 12:9-12, 20:10 **2** Eze. 33:12-13, 18, Lk. 9:23, 62, Mdo. 14:22, Rum. 11:22, Efe. 6:10-18, 1 Thes. 5:22, 2 Thes. 2:13-15, 1 Tim. 4:16, 6:12, Ebr. 3:12-14, 1 Pet. 1:13-17, 2 Yoh. 8 **3** Isa. 30:33, Mat. 13:24-30, 37-43, 47-50, Mk. 9:43-48, Lk. 3:17, 16:19-31, Ebr. 10:26-31, Ufu. 14:9-11, 19:20, 20:10-15, 21:8 **4** Mit. 6:22-23, Mat. 4:3-11, 8:16, Yoh. 8:31-32, 14:6, 17:17, 2 Tim. 3:14-17, Ebr. 4:12, Yak. 1:21-22

# USHINDI DHIDI YA PONOGRAFIA!

*(Inaendelea kutoka ukurasa wa 1)*

Daudi aliyatenda haya na kama sio hivyo hangesema:] Kwa midomo yangu nimezisimulia hukumu zote za kinywa CHAKO. Nimeifurahia njia ya SHUHUDA ZAKO kana kwamba ni mali nyingi. [Kutoroka nguvu ovu za mawazo machafu ya ngono na mawazo yaliyobuniwa ya ngono ni kutenda alivyotenda mzaburi Daudi.] Nitayatafakari mausia YAKO, nami nitaziangalia njia ZAKO. Nitajifurahisha sana kwa amri zako SITALISAHAU NENO LAKO" (Zaburi 119:9-16).

Afueni kutoka kwa tamaa zoea za mwili, kutokana na mawazo machafu ya ngono, kutokana na uovu, hali ya kugandamiza ya ponografia na uhalifu wa kila aina ya ngono inahitaji mtu kuweka akili safi, ambayo inawezekana tu kwa kutafakari kila wakati juu ya NENO la MUNGU![5] Ukombozi kutoka kwa pombe, dawa za kulevya na dhambi zote hupatikana kwa njia hiyo hiyo; kwa NENO LA MUNGU!

Kuwa mwaminifu kwa mke au mume wako wakati yeye hayupo karibu na kuponya majeraha ya uzoefu wa uzinzi hupatikana TU kwa akili safi iliyooshwa na NENO la MUNGU; ambayo imejijaza uponyaji, tumaini na afueni kutoka kwa uzoefu wa ngono; ponografia.[6] Unafaa kupambana na jambo hili kila siku. "Tukiangusha [kwa NENO la MUNGU] mawazo na kila kitu kilichoinuka, kijiinuacho juu ya elimu ya MUNGU na tukiteka nyara kila fikira ipate kumtii KRISTO [kunyenyekea chini ya NENO la MUNGU]" (2 Wakorintho 10:5).

Zaburi 119:1-3 (ALEFI): "Heri walio kamili katika njia zao, waendao katika SHERIA ya BWANA. [Shetani ambaye huleta mawazo ya picha mbaya za uchi ndiye shetani akuambiaye kuwa sheria na maadili ya MUNGU imemalizika![7] Huu ni UONGO, kama vile ni uongo wa Shetani wakati anakuambia ya kwamba unapata faida fulani kutokana na ponografia. YESU alisema, 'Msidhani ya kuwa nimekuja kutangua SHERIA, au manabii: La, sikuja kutangua, bali kutimiliza. Kwa maana, amin, nawaambia, Mpaka Mbingu na nchi zitakapoondoka, yodi moja wala nukta

**5** Yos. 1:8, Zab. 1:1-3, 19:7-11, 63:5-6, 119:48, 55, 97, 148, 143:5, Mit. 3:1, 6:20-23, 23:12, Mat. 4:4, Lk. 11:28, Yoh. 8:31-36, 15:3-7, 17:17, Mdo. 20:32, Efe. 5:25-27, Kol. 3:16, 2 Tim. 2:15, Yak. 1:21-22, 1 Yoh. 2:14 **6** Isa. 26:3-4, Mat. 5:6, Yoh. 6:63, 14:23-24, 15:3, Kol. 3:1-2, 16 **7** Zab. 111:7-8, 119:89, 152, 160, 138:2, Mhu. 3:14, Isa. 24:5, 40:8, Yer. 31:31-33, Mat. 5:17-48, Mk. 13:31, Lk. 10:25-26, Rum. 3:31, Ebr. 10:16, 13:8, Ufu. 22:18-19

# Barua za Pastor Alamo

## Italia

Ndugu Mchungaji Tony Alamo,

Kwa mara nyingine tena, namshukuru Mungu kwa maisha yako na huduma.

Mchungaji, ninawashukuru kwa ajili ya zawadi yako ya hivi karibuni yenye dhamani: Biblia, vitabu vya Masihi na nakala ambazo ulituma kwangu. Mimi nina fahari kuwa mwanachama wa familia hii ya ajabu na utukufu wa Mungu.

Mchungaji Alamo, kwa neema ya pekee ya Bwana wetu Yesu Kristo, na kwa msaada wa maombi yako na vitabu fasihi, Bwana ameniita kuwa mtumishi wake; na kwa neema yake maalum, mimi nimekusanya idadi kubwa kabisa ya watu. Kwa hiyo naomba ruhusa yako ya kufanya kazi chini ya huduma yako. Katika hili niupe ushirika huu jina la huduma yako, na utakuwa baba yangu moja kwa moja kiroho. Nina matumaini ya kusikia kutoka kwenu haraka iwezekanavyo.

Jambo la kweli ni kwamba, vitabu vyako vimekuwa vya Baraka sana hasa Italia. Hapo awali, wengi wao walisita kukubali maandiko wakati yalipokuwa yakitolewa kwao. Hata hivyo, kwa muda na sala, usambazaji sasa unasonga mbele vizuri kukiwa na upinzani mdogo sana.

Mchungaji, katika mtazamo huu, napenda kuomba vitu vifuatavyo: Biblia mbili Takatifu katika lugha ya Italia, Redio ndogo ya kurekodi mkanda na mikanda ya video katika lugha ya Kiingereza. Natumaini kwa nguvu ya Roho Mtakatifu, vitabu vyako vilivyopakwa mafuta vitafungua macho ya Waitaliano wengi na kuwaleta wengi katika ufalme wa Mwana mpendwa wa Mungu, Yesu.

Mimi bado wako mwaminifu,
Mchungaji BK Sakyi
Ghedi, Italia

## Arkansas

Ndugu Tony,

Mheshimiwa, mimi nilitaka kuandika na kuwaambia kwamba maandiko yamekuwa ya ajabu sana na yenye msukumo mkuu, yaliyojawa na Mungu, yaliyojawa na mafundisho, matumaini, ukweli na furaha! Mimi namtukuza Mungu kwa ajili yao na wewe!

Maandiko yako daima yametiwa pumzi ya Mungu, lakini yanazidi kuwa bora zaidi na zaidi kwa kila kipande cha maandiko. Hatuwezi kusubiri barua ili tuweze kusoma pamoja. Zako ni za ajabu.

Sisi sote tunakupenda na kukukosa sana.

V.L. Texarkana, AR



**HUDUMA YA MTANDAO YA ALAMO**
**www.alamoministries.com**

moja ya torati haitaondoka, mpaka yote yatimie' (Mathayo 5:17-18). Shetani hapendi wewe uamini katika nguvu za ukombozi katika NENO la MUNGU, lakini jaribu jambo hili na utaona kwamba NI KWELI!] Heri wenye kuweka shuhuda ZAKE na WAMFUATAO kwa moyo wote. Wao pia hawatendi uovu bali wanatembea katika njia ZAKE."

Shetani ataweza, ikiwa utamruhusu, kuleta kumbukumbu ya zamani ya ngono akilini mwako. Wakati huo ndio unaofaa kupambana naye papo hapo kwa NENO la MUNGU. Tafuta Biblia yako KJV, [toleo la Kiswahili la The Bible League, waenezaji wa Neno la Mungu tangu mwaka wa 1938] na uanze kusoma ZABURI hapo hapo. Usisubiri. Shetani anatafuta nafsi yako. Katika vita, ikiwa unatupiwa risasi, lazima urushe yako pia. Shetani anakutupia risasi, nawe unastahili kumtupia yako pia ukitumia NENO la MUNGU.[8] "(Maana silaha za vita vyetu si za mwili, bali zina uwezo [KIROHO] kwa njia ya MUNGU hata kuangusha ngome;) tukiangusha mawazo na kila kitu kilichoinuka, kijiinuacho juu ya elimu ya MUNGU na tukiteka nyara kila mawazo ya utii wa KRISTO" (2 Wakorintho 10:4-5).

Shetani yule yule ambaye anakutupia mishale ya moto ya ponografia anakwambia kwamba NENO la MUNGU halifanyi kazi na kwamba SHERIA ya MUNGU, SHERIA ya maadili, si lazima izingatiwe kwa sababu haina ukweli wowote tena. Huyu ndiye shetani yule yule ambaye anakusingizia wewe, kukushutumu kwa njia ya uongo, na pia, kumsingizia MUNGU. Tunafaa kukumbuka kwamba yeye ni mwongo na baba wa waongo wote na ni lazima kupigana naye (Yohana 8:44).

BIBLIA ya KJV inasema kwamba sisi tu katika vita. Hii ina maana kuwa sisi lazima kupambana kwa njia ya halali, tukitumia NENO la MUNGU.[9] Shetani anaiambia dunia nzima kwamba MUNGU tayari ameshughulikia mambo yote, kumaanisha kwamba sisi hatutakiwi kufanya kitu chochote kamwe! Huu ni uongo. Sisi tutahukumiwa kwa MATENDO yetu.[10] Soma kitabu cha Yakobo na hata Biblia nzima.

Je, sisi tunafaa kumheshimu MUNGU kivipi? Je, sisi tunadhibitisha UPENDO wetu KWAKE vipi? "MKINIPENDA, mtazishika amri ZANGU"

*(Inaendelea ukurasa wa 4)*

**8** 2 Kor. 10:3-6, Efe. 6:10-18, 1 Tim. 6:12, Yak. 4:7, 1 Pet. 5:8-9 **9** Mat. 26:52, 2 Kor. 10:3-6, Efe. 6:10-18, Flp. 1:27-30, 1 Tim. 6:12, 2 Tim. 2:3-5, Ebr. 4:12, 1 Yoh. 2:13-17, 4:3-4, 5:4 **10** Mwa. 17:1, 26:4-5, Kut. 15:26, Law. 22:31, Hes. 15:40, Kum. 4:2, 40, Ayu. 34:11, Isa. 56:1-2, Eze. 3:17-21, 33:1-9, Mat. 25:31-46, 1 Kor. 3:9-17, Gal. 6:7-9, 2 Tim. 4:5-8, Tit. 2:11-14, Yak. 2:12-26, 1 Pet. 1:17, Ufu. 3:2, 15-19, 20:12-13

## Ufilipino

Ndugu Mwinjilisti Tony Alamo,

Mimi ni mtu ambaye huwasha tu radio wakati ambapo nataka kusikiliza muziki. Mimi nina uzoefu wa kusikiliza muziki wa classic. Siku moja, rafiki aliniambia kuhusu kipindi chako na jinsi yeye alikuwa amefunguliwa macho. Nilimsikia na nikaweza kusikiliza kipindi chako. Tangu wakati huo, uchaguzi wangu wa kusikiliza umeleta mabadiliko katika maisha yangu.

Kusikiliza kipindi chako kwa namna fulani hunipa msukumo na nimezidi kujua zaidi kuhusu Bwana wetu Yesu Kristo. Nimekuwa nikisikiliza kwa makini zaidi tangu wakati nilipokuwa Mkristo na ninazidi kujua maana haswa ya neno.

Wewe ni kiongozi wangu wakati mimi naomba. Maneno hayatoshi kukushukuru.

Mungu akubariki.

Virginia J. Torio — Pandacan, Manila, Ufilipino

## Kenya

Nina msisimko sana kuwaambia kwamba mwishowe, nimekumkubali Yesu Kristo kama Mwokozi wangu binafsi na kwamba alikufa juu ya msalaba. Baada ya kusikiliza kipindi chako, sasa ninajua kwamba nilikuwa nimepotea lakini Bwana amenileta katika mwanga.

Mwenyezi Mungu akubariki kwa kazi nzuri unayoifanya.

Tafadhali nitumie baadhi ya magazeti yaliyojaa tumaini ya Kikristo.

Mimi ni wako katika Kristo,

Annribah Gaceri — Meru, Kenya, Africa

## Uganda

Ndugu Mchungaji Tony Alamo,

Hongera kwa kazi nzuri ambayo wewe pamoja na huduma yako mnaifanya. Mimi nilipokea barua yako kutoka kwa rafiki katika Kasese, mji wa Uganda. Niliitafsiri katika lugha yetu (ya ndani) yaani (Lukonjo), ili kuwasaidia wale ambao hawawezi kusoma Kiingereza. Barua yako imekuwa rasilimali yangu bora wakati niko nje kwa uinjilisti. Wengi waliopotea wamemkubali Yesu Kristo na maisha ya watu wengi yamebadilika.

Tafadhali nitumie barua nyingi unavyoweza pamoja na Biblia. Kanisa ninalochunga pamoja na watoto wa shule (Shule ya Bweni ya Little Angels ambapo mimi hutumika kama mchungaji) wanaziitaji.

Asante sana kwa majibu yako. Mwenyezi Mungu akupe malipo kwa ajili ya kazi nzuri.

Wako katika huduma yake,

Mchungaji Kule Expedito mchungaji mkuu, shule za bweni za Little Angels
Kasese, Uganda, Afrika

## USHINDI DHIDI YA PONOGRAFIA!

*(Inaendelea kutoka ukurasa wa 3)*

(Yohana 14:15). "Yeye anayesema, namjua YEYE, na <u>HAZITENDI</u> amri ZAKE, ni mwongo, na UKWELI [KRISTO] HAUMO ndani yake" (1 Yohana 2:4).

Ungama dhambi zako kwa MUNGU na kutubu kwa kusema sala hii:

**BWANA wangu na MUNGU wangu, ihurumie roho yangu, mimi mwenye dhambi.[11] Ninaamini kwamba YESU KRISTO ni mwana wa MUNGU aliye hai.[12] Ninaamini kwamba alikufa msalabani na kumwaga damu yake ya thamani ili nisamehewe dhambi zangu zote nilizozifanya hapo awali.[13] Ninaamini kwamba Mungu alimfufua YESU kutoka kwa wafu kupitia nguvu za ROHO MTAKATIFU[14] na ya kuwa ameketi upande wa kuume wa MUNGU kwa wakati huu akisikiliza maungamo ya dhambi zangu na haya maombi yangu.[15] Ninafungua mlango wa moyo wangu na kukukaribisha moyoni mwangu, BWANA YESU.[16] Nioshe dhambi zangu kwa damu uliyoimwaga kwa ajili ya nafsi yangu pale msalabani Kalivari,[17] hutanikataa, BWANA YESU, utanisamehe dhambi zangu na kuiokoa roho yangu. Ninalijua hili kwa sababu NENO LAKO, yaani Biblia linasema hivyo.[18] NENO LAKO linasema hutamkataa yeyote na mimi nikiwemo.[19] Hivyo ninajua umenisikia na umenijibu; na ninafahamu kwamba nimeokoka.[20] Ninakushukuru BWANA YESU kwa kuokoa roho yangu na nitaonesha shukrani zangu kwa kufanya yale unayoniamuru na kwa kutotenda dhambi tena.[21]**

Baada ya kuokoka, YESU alisema kuwa ni lazima kubatizwa kwa kuzamishwa kabisa kwenye maji mengi kwa jina la BABA, MWANA na ROHO MTAKATIFU.[22] Kwa makini, soma Biblia ya KJV, tafsiri ya Kiswahili ya The Bible League, Waenezaji wa Neno la Mungu tangu 1938 na ufanye inavyosema.[23]

BWANA anakutaka uwaambie wengine kuhusu wokovu wako. Unaweza kusambaza makala ya Injili ya mchungaji Tony Alamo. Tutakutumia makala hizi bila malipo. Tupigie simu ama ututumie barua pepe kwa habari zaidi. Mshirikishe mtu mwingine na ujumbe huu.

Iwapo unataka dunia yote, iokolewe kama YESU anavyoamuru, basi usimwibie MUNGU zaka na sadaka zake. MUNGU alisema, "Je! Mwanadamu atamwibia Mungu? Lakini ninyi mnaniibia mimi. Lakini ninyi mwasema, Tumekuibia kwa namna gani? Mmeniibia zaka na dhabihu. Ninyi mmelaaniwa kwa laana; maana mnaniibia mimi, naam, taifa hili lote [na dunia hii yote]. Leteni zaka [zaka ni asilimia 10 ya mapato yako yote] kamili ghalani, ili kiwemo chakula [chakula cha kiroho] katika nyumba yangu [roho zilizookolewa], mkanijaribu kwa njia hiyo, asema Bwana wa majeshi; mjue kama sitawafungulia madirisha ya mbinguni, na kuwamwagieni baraka, hata isiwepo nafasi ya kutosha, au la. Nami kwa ajili yenu nitamkemea yeye alaye, wala hataharibu mazao ya ardhi yenu; wala mzabibu wenu hautapukutisha matunda yake kabla ya wakati wake katika mashamba, asema Bwana wa majeshi. Na mataifa yote watawaiteni heri; maana mtakuwa nchi ya kupendeza sana, asema Bwana wa majeshi" (Malaki 3:8-12).

**11** Zab. 51:5, Rum. 3:10-12, 23 **12** Mat. 26:63-64, 27:54, Lk. 1:30-33, Yoh. 9:35-37, Rum. 1:3-4 **13** Mdo. 4:12, 20:28, Rum. 3:25, 1 Yoh. 1:7, Ufu. 5:9 **14** Zab. 16:9-10, Mat. 28:5-7, Mk. 16:9, 12, 14, Yoh. 2:19, 21, 10:17-18, 11:25, Mdo. 2:24, 3:15, Rum. 8:11, 1 Kor. 15:3-7 **15** Lk. 22:69, Mdo. 2:25-36, Ebr. 10:12-13 **16** 1 Kor. 3:16, Ufu. 3:20 **17** Efe. 2:13-22, Ebr. 9:22, 13:12, 20-21, 1 Yoh. 1:7, Ufu. 1:5, 7:14 **18** Mat. 26:28, Mdo. 2:21, 4:12, Efe. 1:7, Kol. 1:14 **19** Mat. 21:22, Yoh. 6:35, 37-40, Rum. 10:13 **20** Ebr. 11:6 **21** Yoh. 5:14, 8:11, Rum. 6:4, 1 Kor. 15:10, Ufu. 7:14, 22:14 **22** Mat. 28:18-20, Yoh. 3:5, Mdo. 2:38, 19:3-5 **23** Kumb. 4:29, 13:4, 26:16, Yos. 1:8, 22:5, 2 Tim. 2:15, 3:14-17, Yak. 1:22-25, Ufu. 3:18

*Tafadhali wasiliana nasi kwa habari zaidi au kwa vitabu vyetu vyenye mada nyingine ambazo unaweza kuvutiwa nazo:*

**Tony Alamo, World Pastor, Tony Alamo Christian Ministries Worldwide • P.O. Box 2948, Hollywood, CA 90078**
**Namba yetu ya simu kwa ajili ya maombi na habari iliyo wazi kwa saa ishirini na nne ni: (661) 252-5686 • Faksi: (661) 252-4362**
**www.alamoministries.com • info@alamoministries.com**

*Huduma ya Tony Alamo Christian Ministries Worldwide hutoa mahali pa kuishi pamoja na vitu vyote muhimu kwa maisha kwa wale walio Marekani ambao wanataka kumtumikia BWANA kwa mioyo yao yote, roho zao zote na nguvu zao zote.*

**Huduma yetu hufanyika jijini New York kila Jumanne, saa mbili usiku na mahali pengine kila usiku.**
**Tafadhali wasiliana nasi kupitia simu namba (908) 937-5723 kwa habari zaidi. CHAKULA HUTOLEWA BAADA YA KILA IBADA.**

**Tuma maombi ujipatie kitabu cha Mchungaji Alamo kiitwacho, The Messiah, kinachomwonesha KRISTO alivyo katika Agano la Kale kwa jumbe za unabii zipatazo 333.**

*Kuwa mmoja wa watumishi katika kuvuna roho za watu kwa kuwa msambazaji wa makala na vitabu vya Mchungaji Alamo*
*Machapisho yetu na jumbe kwenye tepu za sauti hayalipishwi kitu ikiwemo gharama ya kusafirisha kupitia meli.*
*Iwapo kuna mtu atajaribu kukulipisha, tafadhali tupigie simu kwa namba: (661) 252-5686.*

**MAKALA HIZI ZIMEBEBA MPANGO WA KWELI WA UKOMBOZI (Matendo ya Mitume 4:12)**
**USIZITUPE: ZIFIKISHE KWA MTU MWINGINE.**

**Kwa wale ambao mko kwenye nchi nyingine, tunawashauri kutafsiri makala hizi kwa lugha zenu. Iwapo mtachapisha tena, tafadhali jumuisha haki hii na usajili:**

© Haki ya Kunakili Oktoba 2011, 2015 Haki zote zimehifadhiwa Mchungaji wa Ulimwengu Tony Alamo® Tarehe ya Usajili Oktoba 2011, 2015

SWAHILI—VOLUME 13600—*VICTORY OVER PORNOGRAPHY!*